# OFISI YA WAZIRI MKUU
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI
## SHULE YA SEKONDARI **KISARAWE II**

S.L.P 36645
Dar es Salaam
Tanzania

Simu+255629961848
+255654532054

**TAREHE: ……/……/ 2026**

---

**KUMB NA ………………………………………………**
**JINA LA MWANAFUNZI ………………………………**
**…………………………………………………………**
**S.L.P……………………………………………………**
…………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISARAWE II ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2026**

**01. Utangulizi**

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) mwaka **2026.** Shule ya **Sekondari Kisarawe II** Ipo umbali wa km **27** toka Ferry Kigamboni. Jinsi ya kufika shuleni, kwa wale wanaoanzia Standi ya Mbezi(Magufuli) wapande mabasi ya mwendo kasi na wateremke **Kivukoni**. Baadae watapanda **Panton** kwa ajili ya kuvuka bahari, Baada ya kuvuka bahari wataenda kituo cha daladala **Kigamboni** na wapande daladala za Kibada na kushuka kituo cha daladala **Kibada**. Baada ya hapo panda daladala za **Mwasonga** na kushuka kituo cha **Kisarawe II**. Na kwa wanaotokea Standi ya Mbagala panda daladala za Mwasonga zinapatikana **Zakheem** na uteremke **SHULE YA SEKONDARI KISARAWE II**.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **………../01/2026** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **…../01/2026**

**02. Mambo muhimu ya kuzingatia**

**03. Sare za Shule kwa Wanafunzi Wasichana**

Sketi ndefu za rangi ya khaki No 1na shati jeupe na wanaovaa Majuba yawe meupe

**Maelezo ya mshono.** Sketi ya rinda boksi ndefu zinazofika vifundo vya mguu na shati za mikono mifupi na kwa wanaovaa hijabu nusu kanzu ziwe nyeupe zinazofika chini ya makalio na ziwe mikono mirefu zisizobana na hijabu **ifunike mikono Pamoja na viganja vyake**, viatu vyeusi vya Kamba na soksi nyeupe

**Mahitaji muhimu kwa wanafunzi Wasichana**

a) Pair mbili za kanga/kitenge
b) Ndoo tatu ndogo, makopo 2 ya kuogea, kikombe cha chai cha plastiki, sahani ya kuwekea chakula(**kolabo**)kijiko cha chai, sabuni ya kufulia, sabuni yakuogea.
c) Sanduku la chuma(trancker), begi la mgongoni kubebea madaftari
d) Shuka za pinki mbili, net 1(chandarua)rangi ya blue, Godoro ya $2^{1/2}$ ,track suit rangi ya blue1, Ream paper 2, Jembe 1 bila ya mpini, T-shirt za shule 4, madaftari 15 counter book(quire 2)

## **Sare za Shule kwa** Wanafunzi **wavulana**

Suruali za kaki No 1 zisizobana na viatu vyeusi vya Kamba visivyo na visigino virefu na sweta la dark blue, soksi nyeusi na mashati meupe ya mikono mifupi.(modo haziruhusiwi)

**Mahitaji muhimu kwa wanafunzi Wavulana**

a) T-shirt za dark blue zisizobana (shamba dress)
b) Ndoo ndogo 3 za kuogea, sanduku la chuma (Trancker), begi la kubebea madaftari
c) Shuka mbili za blue, net 1(chandarua), Ndoo ndogo 3, makopo yakuogea 2, kikombo cha chai cha plastick, sahani ya kuwekea chakula(**kolabo**), kijiko cha chai, sabuni ya kufulia, sabuni ya kuogea.
d) Ream paper 2, jembe 1, T-shirt za shule 4, Madaftari 15 counter book(quire 2), Godoro $21^{1/2}$, Track suit rangi ya blue1, T-shirt ya michezo rangi ya blue 1 na bukta yake na Jembe 1

**ZINGATIA,** vifaa tajwa hapo chini vinapatika katika maduka ya Jirani na shule hivyo unashauriwa kuja nunua kwenye maduka hayo kama mchanganuo wa bei unavofuata ili kuepuka kubeba mizigo mingi. (Hii ni kwa watakaohitaji huduma hii Jirani na shule)

i. T-Shirt za shule Tsh 15,000 kwa kila moja
ii. Ndoo za kuogea Tsh 5,000 kwa kila moja
iii. Godoro Tsh 50,000
iv. Track suit Tsh 25,000 kwa kila moja
v. Ream paper Tsh 15,000 kwa kila moja
vi. Shuka Tsh 10,000 kwa kila moja

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na 10** ya mwaka **1995.** Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi , yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAISI –TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima,
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima ,
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation kwa bweni)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii,
f) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ; na
i) Kutunza mali za umma

## 3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji

Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

Kupigana au kupiga

d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
e) Kudharau Bendera ya Taifa
f) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba
g) Kuoa au kuolewa
h) Kutoa mimba
i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
j) Kukataa adhabu kwa makusudi

k) Kuwa na simu ya mkononi

**4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

a) Medical Examination form ambayo itajazwa **na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali** . Fom**u hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara** utakaporipoti shuleni
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo , fujo na makosa ya jinai
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

**MUHIMU:**

Mzazi unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu vya masomo ya darasani (vitabu vya kiada ) vilivyo chapishwa na **Taasisi ya Elimu Tanzania (T .I . E) / Tanzania Institute of Education au vitabu vilivyo chapishwa na Oxford pia Kamusi na Oxford Dictionary (English-English) ni muhimu sana kwa mwanafunzi .**

**Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na BIMA YA AFYA kwa wasiokuwa na bima ya afya mzazi unatakiwa kumlipia mwanafunzi kwa gharama ya Tsh 50,400. Bima ya Afya kwa wanafunzi wa bweni ni lazima ilikuepusha usumbufu wa gharama za matibabu kwa mzazi. Fedha za Bima lipa kupitia NMB, Akaunti namba 22403300001 jina la Akaunti SCHOOL FUND ACCOUNT, KISARAWE II.**

**N.B:** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KISARAWE II SEKONDARI**

…………………………

**FLORENTIN F ASSENGA.**

**MKUU WA SHULE**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE NA AHADI YA KUTII NA KUFUATA KIKAMILIFU**

**SHERIA NA TARATIBU ZOTE ZA SHULE**

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KISARAWE II,
S. L. P 36645,
**DAR ES SALAAM.**

**KWA MWANAFUNZI**

7nafasi niliyopewa kujiunga na Kidato cha ……………..….mwaka…………..katika Shule ya Sekondari Kisarawe II.

**NINAAHIDI KWAMBA;**

1. Nitatii sheria zote za Shule hii kama nilivyosoma katika fomu ya kujiunga na Shule.
2. Nitakuwa na bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za Shule.
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyo bora bila kuitia hasara Shule kwa uharibifu au upotezaji wa malighafi ( Raw Materials za Uzalishaji Mali).
4. Nitakuwa Mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, Mkakamavu na Mwenye mwenendo safi wakati wote hata nikiwa nje ya mipaka ya Shule kwa dhumuni la kuipa nakutunza sifa ya Shule ya Sekondari ya………………………..

**MUNGU NISAIDIE**

Saini ya Mwanafunzi …………………………………………………..Tarehe ………………

**KWA MZAZI / MLEZI**

Mimi ……………………………………………………………………(Jina Kamili la Mzazi / Mlezi)

**NINAAHIDI KWAMBA;**

1. Nitampatia Mwangu mahitaji yake yote ya Shule kama yalivyotajwa katika maelezo ya kujiunga na Shule.
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote ule utakao hitajika ( Maoni, Adhabu) katika kumlea Mwanangu.
3. Nitamuhimiza Mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo ya nyumbani (Home Work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake Shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza vizuri na kumwangalia vizuri mwenendo wake wa kila siku.

Saini ya Mzazi/ Mlezi…………………………………………………

Tarehe………………………

# SHULE YA SEKONDARI KISARAWE II
# FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI

A: **MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi ……………………………………………………….
2. Tarehe ya kuzal iwa ………………………………………………………………..
3. Utaifa………………………………………………………………………………
4. Uraia ……………………………………………………………………………
5. Dini…………………………………………………………………………………
6. Shule ya msingi aliyo soma ………………………………………………………………

Jina la shule ya msingi aliyotoka mwanafunzi ………………………tarehe ya kuanza shule……………

Tarehe aliyomaliza shule ………………………………………………………………………

Sahihi ya mwanafunzi………………………………………….. tarehe …………………………………

B: **MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la mzazi ………………………………………………… 2. Utaifa ……………………………………………………………… 3. Uraia ………………………………………………………………
4. Anuani ya kudumu ……………………………………………………
5. Sehemu anakoishi …………………………………………………..
6. Mtaa ………………………Kata…………………………………..
7. Namba ya nyumba ……………………………………………………
8. Barua pepe…………………………………………………………

a. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi……………………………………………
   Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………………
b. **Namba ya simu ya mtu wakaribu…………………………………………………….**
   **Jina…………………………………………………Uhusiano……………………………….**
c. **Namba ya simu serikali ya mtaa/Kijij/Mwenyekiti/Mtendaji……………………..**
   **Taja mtaa/Kijiji……………………………………Wilaya……………………………………..**

Eleza kama mtoto wako ana matatizo ya kiafya
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

**C: MAELEZO YA KIKAZI**

1. Jina la mwajiri …………………………………………………… ………………
2. Anuani ya mwajiri ……………………………………………………………
3. Kazi ya mzazi/mlezi. (mf.Ka rani ,mwalimu)……………………………………

Sahihi ya mzazi/mlezi ……………………………………………………tarehe …………………

**KIGAMBONI MUNICIPAL COUNCIL KISARAWE II SECONDARY SCHOOL**

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be filed by the Government Medical Officer and return back to the HEAD OF KISARAWE II
SECONDARY SCHOOL P.O. BOX 36645 Dar es Salaam
To the Medical
………………………………………………..
……………………………………………….. …………………………………………………

A Re ………………………………………………………………………………..
Please, examine the abovementioned student and comment on his/her fitness by responding to the problems below Say YES or NO each problem and if yes then STATE
**HEADMISTRESS DATE…………………………**

Insert (√) in the boxes provided

i. Hearing YES ( ) NO ( )
ii. Speech YES ( ) NO ( )
iii. Sight YES ( ) NO ( )
iv. T.B YES ( ) NO ( )
v. B.P YES ( ) NO ( )
vi. Diabetes YES ( ) NO ( )
vii. Physical liability YES ( ) NO ( )
viii. Mental Care YES ( ) NO ( )
ix. Any other ( )
…………………………………………………………………………………………………….
x. States…………………………………………………………………………………………………..

B: Recommend if the student fits for studentship (i) YES (ii) NO
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
C: Any other advice ………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………………….. Name and Signature ………………………………………………………………Title ……………………………..

**STAMP**